**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA SABA

## KIKAO CHA HAMSINI NA MOJA

**20 JUNI, 2017**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA SABA

## KIKAO CHA HAMSINI NA MOJA – TAREHE 20 JUNI, 2017

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**416. MHESHIMIWA RHODA EDWARD KUNCHELA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Pamoja na lengo la Serikali kuhakikisha Manispaa zinakuwa safi na kuzuia magonjwa ya mlipuko, Manispaa ya Mpanda ina changamoto ya ukosefu wa vifaa kama magari ya taka:-

Je, Serikali ina mikakati gani wa kuhakikisha Manispaa zinakuwa safi .

## WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

### 417. MHESHIMIWA RICHARD PHILIP MBOGO (NSIMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- *Electronic Fiscal Device (EFD)* risiti hazidumu kwa muda mrefu kwani zinafutika maandishi ndani ya muda mfupi:-

Je, TRA wataridhika na maelezo ya mlipa kodi bila ushahidi wa risiti.

## WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

### 418. MHESHIMIWA AMINA SALEH MOLLEL (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo :- Haki ya kupata taarifa ni Haki ya msingi kwa kila Mtanzania na Vyombo vyetu vya Habari havina Wakalimani wa lugha ya alama kwa ajili ya kuwawezesha Viziwi kupata habari kwa uelewa uliotimilifu kama raia wengine:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa Vyombo vya Habari hasa TV vinaajiri Wakalimani hasa katika taarifa za habari ili waweze kufuatilia matukio yanayooneshwa.

**419. MHESHIMIWA BALOZI ADADI MOHAMED RAJAB (MUHEZA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:- Mawasiliano ya TBC (Redio) kwenye maeneo ya Tarafa ya Amani – Muheza ni hafifu:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha mawasiliano ya Redio na TV ya kituo cha Taifa cha TBC;

(b) Je, ni lini Serikali itaboresha mawasiliano kwenye maeneo hayo ya milima ya Amani ya vituo vya Taifa Redio na TBC ili Wananchi waweze kunufaika na vipindi hivyo.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**420. MHESHIMIWA RAISA ABDALLAH MUSSA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Wapo Wanawake ambao wamefungwa Magerezani wakiwa na Watoto wachanga/ wadogo ambao bado wanahitaji uangalizi au huduma za Mama zao:-

(a) Je, Serikali imejipanga vipi katika kuwanusuru Watoto hao ambao hawana hatia;

(b) Je, Serikali haioni kuwa inavunja Haki za Binadamu kwa kuwaweka Magerezani Watoto hao wasio na makosa;

(c) Je, Serikali inaweza kulipa Bunge takwimu za Wanawake waliokinzana na Sheria na wamefungwa kwa miaka mitano iliyopita.

**421. MHESHIMIWA ELIAS JOHN KWANDIKWA (USHETU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Miaka ya hivi karibuni kumekuwepo na mauaji ya Wazee na Walemavu wa ngozi kutokana na sababu mbalimbali:-

(a) Je, ni idadi ya watu wangapi waliopoteza maisha katika Jimbo la Ushetu kwa kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015;

(b) Je, Mauaji ya makundi haya yanapungua au yanaongezeka katika Jimbo la Ushetu;

(c) Je, Serikali imeshirikisha vipi Jamii kupiga vita mauaji haya, vikiwemo vikundi vya Dini, walinzi wa jadi (sungusungu) na uongozi wa kimila Jimboni Ushetu.

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

### 422. MHESHIMIWA DKT. DAVID MATHAYO DAVID (SAME MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Mkomazi Game Reserve (sasa Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi) ilianzishwa kabla ya Uhuru wakati kukiwa na idadi ndogo ya watu na mifugo:-

Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kusogeza mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi ili wananchi wa Kata za Visiwani, Mji Mdogo wa Same na Vumari wapate maeneo ya kuishi, kilimo na ufugaji.

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

### 423. MHESHIMIWA PROF. NORMAN ADAMSON SIGALA KING (MAKETE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Chuo cha Ufundi VETA katika Wilaya ya Makete hakina Mabweni hivyo kunufaisha Kata moja tu wakati Watoto wanaotoka Tarafa za Matamba, Kuwo, Magoma, Bulongwa, Ukwama na Kata za Lupilo na Tandala hawawezi kunufaika na Chuo hicho kwa sababu ya umbali uliopo:-

Je, ni lini Serikali itakipa Chuo hicho kipaumbele cha kukijengea Mabweni.

## WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

**424. MHESHIMIWA SAED AHMED KUBENEA (UBUNGO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Serikali imetangaza kukabidhi rasmi kazi ya kufufua Kiwanda cha kutengenza tairi cha Arusha kwa Shirikia la Maendeleo la Taifa (NDC) baada ya kusitisha rasmi uzalishaji mwaka 2009:-

Je, mpaka sasa kazi ya kufufua Kiwanda hicho imefikia wapi na inatarajiwa kugharimu fedha kiasi gani.

## WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

**425. MHESHIMIWA STEPHEN HILLARY NGONYANI (KOROGWE VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Serikali ilitenga Sh. Bilioni 13 kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa la Mkomazi lakini baadaye Serikali ilihamishia fedha hizo Mkoa mwingine:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurudisha pesa hiyo ili Bwawa lililokusudiwa lijengwe.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge likubali kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

***(Majadiliano yanaendelea)***

## IV. MUSWADA WA SHERIA WA SERIKALI:

***(Kusomwa Kwa Hatua zake zote)***

Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2017 *(The Appropriation Bill, 2017).*

**DODOMA** — **DKT. T. D. KASHILILAH**
**20 JUNI, 2017** — **KATIBU WA BUNGE**